

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: "**TUME**"

DODOMA

Nambari ya Simu: 0738 166 703

0733 005 974

Barua pepe: secretary@psc.go.tz

Tovuti: www.psc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Umma,

Jengo la Chimwaga (UDOM),

Ghorofa ya Pili,

2 Barabara ya UDOM,

S.L.P. 1074,

40405 DODOMA.

Kumb. Na: LA.218/247/01/43

22 Desemba, 2023

TAARIFA KWA UMMA

UTANGULIZI:

Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) ni Idara ya Serikali inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais, iliyoundwa kwa Mujibu wa Kifungu cha 9 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

Jukumu Kuu la Tume ni Urekebu (Regulatory body), ushauri na ushughulikiaji wa Rufaa na Malalamiko ambapo inahakikisha kuwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozi mbalimbali iliyopo katika Utumishi wa Umma.

Kwa Mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) pamoja na Kanuni (60)(1)-(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 vinabainisha Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma kuwa:-

- (i) Tume ya Utumishi wa Umma (PSC)
- (ii) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 10(1) (d) na (g) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) kimeipa Tume, Mamlaka ya kupokea na Kushughulikia Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma mtawalia ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Nidhamu.

Tume katika kutekeleza jukumu hili, kuanzia tarehe 27 Novemba, 2023 hadi 15 Desemba, 2023 Jijini Arusha, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Jaji Mst. Hamisa Hamis Kalombola pamoja na Makamishna 6, ilifanya Mkutano wa pili wa mwaka 2023-2024 kupitia Rufaa na Malalamiko yaliyowasilishwa mbele yake.

Katika Mkutano huo, jumla ya Rufaa na Malalamiko 180 yaliwasilishwa na kutolewa uamuvi katika mchanganuo ufuatao:-

- (i) Rufaa 155 zilisikilizwa na kutolewa uamuvi,
- (ii) Malalamiko 24 yalisikilizwa na kutolewa maamuvi, na
- (iii) Rufaa 1 ilahirishwa kutokana na sababu za kiufundi.

Katika Mkutano huo wa pili wa Mwaka 2023-2024, makosa makubwa yaliyoonekana kutendwa zaidi ni:

- (i) Utoro kazini,
- (ii) Wizi, na
- (iii) Ukosefu wa uaminifu/ukiukwaji uvunjifu wa Maadili ya Utumishi wa Umma.

Aidha katika eneo la Rufaa yafuatayo yalijitokeza:

- (i) Rufaa zilizokubaliwa zilikuwa 14,
- (ii) Rufaa zilizokubaliwa kwa masharti 22,
- (iii) Rufaa zilizokataliwa 78, na
- (iv) Rufaa zilizoletwa Tume zikiwa nje ya muda 27.

Katika eneo la Malalamiko, yaliwasilishwa malalamiko 24 ambayo yalifanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

- (i) Malalamiko yaliyokubaliwa yalikuwa ni 4,
- (ii) Malalamiko yaliyokubaliwa kwa masharti 5, na
- (iii) Malalamiko yaliyokataliwa 15.

Katika Mkutano huo uliofanyika Jijini Arusha, Tume ilipitia Maombi ya Rufaa na Malalamiko yaliyoletwa nje ya muda 14, kati ya hayo, mawili (2) yalikubaliwa na maombi 12 yalikataliwa kwa kukosa sababu za msingi za kusikilizwa nje ya muda.

Aidha, katika Mkutano huo, Tume ilisikiliza warufani 9 kati ya 10 waliokuwa wameomba kufika mbele ya Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za

Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 na mrufani 1 hakufika kwa sababu zake mwenyewe. Pia mrufaniwa mmoja aliomba kufika mbele ya Tume na alifika.

Tume inaendelea kuwakumbusha Watumishi wa Umma kuzingatia Sheria ili kujiepusha na vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa maadili, hali inayoweza kusababisha Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu kuwachukulia hatua za nidhamu au jinai.

Ni muhimu pia kwa Mamlaka za Nidhamu kuzingatia Sheria wakati wa kushughulikia malalamiko ya Watumishi na mashauri ya nidhamu ili haki si tu itendeke bali ionekane inatendeka. Tume inatoa rai kwa Watumishi na Mamlaka za Nidhamu kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma ili kujenga nidhamu na kuleta tija maeneo ya kazi.

Imetolewa na:

Mathew M. Kirama

KATIBU

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

22/12/2023